**HOTUBA YA MHE. JERRY SILAA (MB), WAZIRI WA MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI WAKATI WA HAFLA YA KUKABIDHI VIFAA VYA TEHAMA KWA SHIRIKA LA POSTA TANZANIA, TAREHE 22 AGOSTI 2025**

- Ndugu Mohamed Abdulla, Katibu Mkuu Wizara ya Mawasiliano na Teknolojia ya Habari;
- Mhandisi Peter Mwasalyanda, Mtendaji Mkuu wa Mfuko wa Mawasiliano kwa Wote;
- Ndugu Macrice Daniel Mbodo, Postamasta Mkuu wa Shirika la Posta Tanzania;
- Wakuu wa Taasisi zilizo chini ya Wizara ya Mawasiliano na Teknolojia ya Habari;
- Wakurugenzi na watumishi wa Wizara ya Mawasiliano na Teknolojia ya Habari;
- Menejimenti na wafanyakazi wa Mfuko wa Mawasiliano kwa Wote;
- Menejimenti na wafanyakazi wa Shirika la Posta Tanzania;
- Ndugu waandishi wa Habari;
- Wageni waalikwa;
- Mabibi na Mabwana.

*Ninawasalimu kwa Jina la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania*

Niungane na walionitangulia kuanza kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutupatia afya njema na kutukutanisha mahali hapa kwa ajili ya kushiriki hafla hii yenye lengo la kukuza Sekta ya Posta nchini.

Leo tunashuhudia makabidhiano ya vifaa vya TEHAMA vikiwemo *Personal Digital Assistants (PDA)*, kompyuta na vifaa vingine, vilivyonunuliwa na Mfuko wa Mawasiliano kwa Wote (UCSAF) na kukabidhiwa kwa Shirika la Posta Tanzania. Kama alivyoeleza Katibu Mkuu, hatua hii ni sehemu ya utekelezaji wa Sera za Serikali na maelekezo ya Wizara yetu ya Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, kuhakikisha taasisi zilizo chini ya Wizara zinashirikiana kwa karibu ili kuharakisha upatikanaji wa huduma bora, nafuu na jumuishi kwa wananchi wote.

**Viongozi, Mabibi na mabwana,**

Napenda kutoa pongezi za dhati kwa UCSAF kwa kazi kubwa mnayoifanya. Tumewaona mkipeleka mawasiliano vijijini, mkiunganisha shule na hospitali, na sasa tunaona jitihada zenu za kuiwezesha Posta kuwa chombo cha kisasa cha utoaji huduma. Huu ni mfano bora wa taasisi ya Serikali inayotekeleza kwa vitendo Sera za Kitaifa.

Hakika UCSAF, mmeonesha mfano wa mshikamano wa kitaasisi kwa kushirikiana na Shirika la Posta Tanzania kuhakikisha rasilimali za taifa zinatumika kuboresha maisha ya wananchi. Huu ndio ushirikiano tunaoutaka katika Taasisi zote zilizo chini ya Wizara hii.

**Mabibi na Mabwana,**

Serikali ya awamu ya sita, inayoongozwa na Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, imeweka wazi msimamo wake kwamba huduma za msingi kama vile huduma za posta, mawasiliano ya simu na intaneti na huduma za kifedha za kidijitali kwa sasa si hanasa tena bali ni haki ya kila Mtanzania. Ndiyo maana leo, tunashuhudia Shirika la Posta Tanzania likipewa nyenzo za kisasa ili litoe huduma bora. Hii itamuwezesha mkulima wa kijijini Geita, mvuvi wa Kisiwa cha Ukerewe na mfanyabiashara wa Kariakoo wote kupata huduma bora, za haraka na salama.

**Mabibi na Mabwana,**

Vifaa hivi si tu kwamba vitaboresha kasi ya usambazaji wa barua na vifurushi, bali vitafungua milango ya huduma mpya kama biashara mtandao, malipo ya kidijitali na hata huduma za Serikali mtandao. Huu ndio mwelekeo wa dunia, na Tanzania haiwezi kubaki nyuma.

Kwa kutumia vifaa hivi, Shirika la Posta Tanzania litakuwa na uwezo wa kufuatilia na kusimamia huduma zake kwa ufanisi mkubwa, kupunguza ucheleweshaji na kuongeza uwazi kwa wateja.

**Mabibi na Mabwana,**

Mfuko wa Mawasiliano kwa Wote na Shirika la Posta Tanzania ni taasisi ambazo zipo chini ya Wizara ninayoiongoza, na zote zinashiriki jukumu la Kisera la kuhakikisha huduma za mawasiliano ikiwemo za posta zinawafikia Watanzania wote bila kujali jiografia wala uwezo wao wa kifedha. Ushirikiano huu unadhihirisha dhamira ya Serikali ya kuondoa vikwazo vya upatikanaji wa huduma za msingi za kidijitali sambamba na Mkakati wa Taifa wa Uchumi wa Kidijitali.

**Mabibi na Mabwana,**

Dunia ya leo ipo kwenye Mapinduzi ya Nne ya Viwanda yaani *Fourth Industrial Revolution*, ambapo inashuhudia mabadiliko makubwa ya namna huduma zinavyotolewa na kupokelewa. Mashirika ya Posta Duniani, kupitia Umoja wa Posta Duniani (Universal Posta Union) na Umoja wa Posta Afrika (Pan African Postal Union), yameweka vipaumbele na kubadilisha utoaji wa huduma za posta kutoka mfumo wa zamani kwenda mfumo wa kisasa wa kidijitali zinazowiana na mahitaji ya soko. Tanzania imeamua kuwa sehemu

ya mapinduzi haya, kwa kuhakikisha wananchi wanapata huduma salama, za kisasa na zenye ushindani kimataifa.

**Mabibi na Mabwana,**

Nisisitize kuwa Shirika la Posta Tanzania litumie vifaa hivi kwa ufanisi na kuhakikisha vinaongeza thamani ya huduma na vinaimarisha uaminifu kwa wananchi. Aidha, UCSAF endeleeni kusimamia miradi inayogusa moja kwa moja maisha ya wananchi na hakikisheni kila uwekezaji unaleta matokeo ya kupimika. Wizara ninayoiongoza itaendelea kutoa miongozo na kuhakikisha uwekezaji huu wa Serikali unaleta matokeo Chanya.

Kwa mshikamano huu, tutaijenga Tanzania yenye huduma za kisasa za posta, zinazokidhi viwango vya Kimataifa, na kumuwezesha kila mmoja wetu kunufaika na fursa hizi za kidijitali. Serikali itabaki thabiti kuhakikisha Sekta ya Posta na Mawasiliano kwa ujumla inaendelea kuwa injini ya maendeleo ya kijamii na kiuchumi.

**Viongozi, Mabibi na mabwana,**

Baada ya kuyasema hayo, sasa niko tayari kushuhudia tukio la kukabidhi vifaa husika.

***Asanteni sana kwa kunisikiliza!***